

HALMASHAURI YA JIJI LA ARUSHA



TANGAZO LA ZABUNI

ZABUNI NA: LGA /003/2013 – 2014/ACC/NC/15

UWAKALA WA MABANGO NA UENDESHAJI TAA ZA BARABARANI

24.03.2017

1. Halmashauri ya Jiji la Arusha inakusudia kupata wakala wa Mabango ya biashara kwenye taa za barabarani kwa kipindi cha mwaka mmoja.
2. Halmashauri ya Jiji la Arusha inapenda kuwaalika watu Binafsi, Makampuni, Mashirika, Taasisi au Vikundi vya watu vilivyosajiliwa kisheria, wenye nia na uwezo wa kufanya kazi hizo kutuma maombi yao.

S/NA	LOT NA	JINA LA BARABARA/MTAA	IDADI YA NGUZO/ TAA	AINA YA MABANGO
1.	LOTI 1	NYERERE ✓	31	Barabara zote zenye alama ya tick (✓) zitawekwa mabanyo yanayowaka {light boxes /Illuminated}
2.		KANISA	34	
3.		HAILE SILASIE	32	
4.		SERENGETI	18	
5.		R/A CLOCKTOWER ✓	6	
6.		R/A KIJENGE ✓	8	
		Jumla ndogo	127	
7.	LOT 2	NJIRO	104	
8.		GENERAL TYRE STRETCH	10	
		Jumla ndogo	114	
9.	LOT 3	SIMEONI	37	
		HAILE SILASIE	32	
		Jumla ndogo	69	
10.		BOMA ✓	19	

11.	LOT 4	INDIA ✓	6	
12.		JOEL MAEDA ✓	12	
13.		GOLIONDOI ✓	13	
14.		R/A GOILIONDOI ✓	4	
15.		MAKONGORO A ✓	6	
16.		FIRE ✓	18	
		Jumla Ndogo	78	
17.	LOT 5	MAKONGORO B	34	
18.		R/A MWENGE	6	
19.		E AC ✓	43	
20.		SWAHILI	12	
		Jumla Ndogo	95	
21.	LOT 6	SOKOINE	144	
22.		UNGA LTD & R/A	34	
		Jumla Ndogo	178	
23.	LOT 7	SOMALI	18	
24.		MAKUA	6	
25.		MAIN BUS STAND ✓	28	
26.		WACHAGA A&B	28	
27.		TOWN STAND BUS ✓	6	
		Jumla Ndogo	86	
28.	LOT8	COLONEL MIDELTONE A & FLORIDA -R/A ✓	25	
29.		NHC,WACHAGA,FR BABU,SOWETO	40	
		Jumla Ndogo	65	
30.	LOT 9	BONDENI,MOSQUE, AZIMIO, WANYAMWEZI, MASAI, MARTINI& WASUKUMA.	41	
31.		WAPARE,LINDI,WASANG U	12	
32.		PANGANI,LIVINSTONE,M TENDENI	7	
33.		SALEY	8	
34.		ZEBEDAYO	8	
		Jumla Ndogo	76	
		JUMLA KUU	856	

3. Mwombaji anaruhusiwa kuomba Lot Zisizozidi (2) mbili,kila "Lot" inajitegemea. Mzabuni hataruhusiwa kuomba "Lot" zaidi ya moja kama zabuni moja, hii ina maana kuwa, ukiomba 'lot' zaidi ya moja,mfano lot 2 utatakiwa kununua makabrasha mawili yaani kila lot na kabrasha lake .

4. Zabuni zitashughulikiwa kwa utaratibu wa ushindani wa kitaifa [National Competitive Bidding] ulioanishwa kwenye Kanuni za Manunuzi-[The Public Procurement – goods, works, non-consultant services and disposal of Public Assets by Tender]. Regulations, 2005 na The Local Government Authorities Tender Boards [establishment and proceedings] regulations, 2007 na iko wazi kwa waombaji wote wa hapa nchini.
5. Waombaji wote wenye nia na uwezo wanaweza kupata taarifa kamili kupitia makabrasha ya zabuni katika ofisi ya Katibu wa Bodi ya Zabuni ya Halmashauri ya Jiji la Arusha, barabara ya Boma S.L.P. 3013, Arusha, kila siku kuanzia saa 3.00 asubuhi hadi saa 9:30 mchana, siku za Jumatatu hadi Ijumaa kuondoa siku za sikukuu zinazotambulika kitaifa kuanzia tarehe ya tangazo hili.
6. Makabrasha ya Zabuni yatapatikana baada ya kulipa ada stahili ya zabuni ambayo ni Tshs 100,000/- . Malipo hayo yanaweza kufanyika kwa fedha taslimu ambapo stakabadhi ya Halmashauri itatolewa ikionesha taarifa muhimu za zabuni husika. Vile vile malipo ya maombi ya zabuni yanaweza kufanyika kupitia akaunti ya Halmashauri ya Jiji la Arusha iliyoko katika Benki ya NMB, tawi la Clock Tower, akaunti ya Jumla [General Fund Account] ya Jiji la Arusha Na 4081200001 na kuwasilisha nakala halisi ya hati ya malipo ya Banki [Bank Pay-in Slip, original copy] na kupata stakabadhi ya Halmashauri kwa zabuni iliyoombwa. Malipo yaliyotolewa kama ada ya maombi ya zabuni hayatarejeshwa.
7. Zabuni zote zifungwe ndani ya bahasha iliyofungwa kwa lakiri [seal], na juu ya bahasha iandikwe maandishi yanayotaja aina ya zabuni, namba ya zabuni na "Lot". Zabuni hizo zipelekwe katika sanduku la zabuni lililoko katika ofisi ya Mkurugenzi wa Jiji (Na. 66) kwa kutumia Anuani ifuatayo:-

**Mkurugenzi wa Jiji,
Halmashauri ya Jiji,
Barabara ya Boma,
S.L.P. 3013, Arusha.**

Muda wa mwisho wa kupokea maombi ya zabuni ni **tarehe 24.04.2017 siku ya Alhamisi saa 4:00 asubuhi**. Maombi yote yatafunguliwa muda mfupi baadaye na kwamba waombaji wote au wawakilishi wao wanaalikwa kuhudhuria ufunguzi wa zabuni ..

8. Halmashauri ya Jiji la Arusha hailazimiki kukubali/ kutokubali kutoa zabuni kwa mwombaji zabuni yeyote kutokana na kigezo cha malipo makubwa/malipo kidogo ya eneo utoaji huduma linaloombewa zabuni.
9. Zabuni zitakazochelewa, sehemu ya zabuni, zabuni za kielektroniki, na zabuni zisizofunguliwa katika tukio la ufunguaji Zabuni, kwa hali yoyote ile zabuni hizo hazitakubaliwa kwa tathmini.

**MKURUGENZI WA JIJI
HALMASHAURI YA JIJI LA ARUSHA**